**STATE HOUSE ZANZIBAR**
**OFFICE OF THE PRESS SECRETARY**

**PRESS RELEASE**

**Zanzibar** **09.01.2018**

**RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amesema kuwa sekta ya habari ni kichocheo kikubwa cha maisha ya mwanaadamu hivyo lazima habari ziandikwe kwa usahihi, kwa ukweli na kwa umahiri wake.**

Dk. Shein aliyasema hayo leo katika ufunguzi wa studio za kisasa za Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC -TV), zilizopo Kikwajuni Mjini Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za miaka 54 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Katika hotuba yake, Dk. Shein alisema kuwa sekta ya habri ni kiungo muhimu katika kuwafahamisha wananchi hatua mbali mbali za maendeleo zinapigwa pamoja na kuwapa elimu na maarifa ya kuwasaidia katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili katika maisha yao ya kila siku.

Alieleza kuwa hiyo ndio sababu ya Mwasisi wa Mapinduzi na Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa miaka ya awali ya Mapinduzi na kwa kutekeleza Sera za ASP, aliamua Zanzibar ianzishe kituo cha Televisheni sambamba na kuimarisha kituo cha redio cha Sauti ya Tanzania Zanzibar.

Alieleza kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi zenye historia ndefu ya sekta ya habari kwa mfano uandishi na uchapaji wa magazeti ulianza mwaka 1875 hatua ambayo iliiwezesha Zanzibar kupata fursa ya kutumia mitambo ya upigaji chapa ya aina mbali mbali kwa awamu na katika maeneo tofauti.

Alieleza kwua mwaka 1886, huduma za upigaji chapa zilianzishwa na gazeti la kwanza Zanzibar lilianza kuchapishwa likiitwa Msimulizi na yakafuatia Samachar, Al-Falaq, Muongozo, Afrika Kwetu, Kipanga, Maarifa na mengineyo.

Na kwa upandec wa redio Dk. Shein alisema kuwa matangazo ya redio hapa Zanzibar yalianza rasmi mwezi Machi mwaka 1951 ambapo matangazo rasmi ya televisheni

hapa Zanzibar yalianza mwezi Januari 1974 ikiwa ni televisheni ya rangi ya mwanzo katika bara la Afrika.

Hivyo, Dk. Shein aliwataka wafanyakazi wa ZBC wawe na malengo na moyo wa kufanya kazi kwani chombo chao kina nguvu huku akitumia fursa hiyo kusisitiza matumizi mazuri ya kiswahili kwa waandishi pamoja na watangazaji wa vyombo vya habari vikiwemo redio na televisheni ya ZBC pamoja na gazeti la Zanzibar Leo.

Alisema kuwa siku hizi kiswahili hakiandikwi vizuri, wala hakitamkwi vizuri, hivyo alisisitiza lugha ya kiswahili ipewe heshima yake katika vyombo vya habari.

Alitoa wito kwa wafanyakazi wote wa ZBC kuvitunza vifaa hivyo vipya na kuwataka kuendelea kufanya kazi kwa umahiri, kupendana wenyewe miongoni wmao na kusaidiana na kuwataka kushindana katika kazi na kuahidi kuwapa tunza iwapo watafanya hivyo alivyoagiza.

Alitoa pongezi kwa Said Salim Baghresa kwa mashirikiano yake aliyotoa kupitia chombo chake cha AZAM pamoja na TBC kwa mashirikiano waliyotoa huku akisisitiza haja ya kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa tasnia hiyo ya habari.

Mapema katika mahojiano aliyoyafanya kituoni hapo, Rais Dk. Shein alieleza kuwa sekta nzima ya habari imefanyiwa mabadiliko makubwa sana na kusisitiza haja ya kuwepo kwa mabadiliko kwani serikali imetoa fedha nyingi hivyo ni lazima zisimamiwe na kuipongeza Wizara ya fedha kwa kusimamia hilo na hatimae kupata mafanikio.

Alisema kuwa ilikuwa ni nia yake na Serikali kuunda taasisi yenye nguvu na uwezo na ndio maana akaiunganisha televisheni na redio na kuifanya kuwa kitu kimoja jambo ambalo sio geni kwani hata hapo siku za nyuma ilikuwemo ZBC ambapo jina sio jipya isipokuwa mwelekeo na malengo ndio mapya na kuitaka ZBC kuengeza nguvu ili wawaelimishe vyema wananchi.

Nae Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Rashid Ali Juma alisema alitoa pongezi kwa Dk. Shein kwa hatua na juhudi zake kubwa za kuviimarisha vyombo vyote vya habari vya Serikali pamoja na kuhakikisha studio za ZBC zinapata vifaa vipya na vya kisasa.

Mapema Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Omar Hassan Omar alieleza kuwa kufuatia kikao cha Rais alichokifanya Ikulu na wafanyakazi wa ZBC pamoja na ziara zake za mwezi Septemba 2016 alipotembelea ZBC Redio, Televisheni pamoja na Shirika la Magazeti ya Serikali wakati ule hali haikuwa nzuri sana kwa majengo, vifaa pamoja na maslahi ya wafanyakazi.

Hivyo kutokana na maelekezo ya Dk. Shein, Katibu Mkuu huyo alieleza kuwa ilionekana haja ya kuhama mfumo wa analogia na kwenda dijitali kwa namna ilivyobora zaidi kama ilivyo kwa TBC na AZAM Media, kupata vingamozi bora na ambavyo vitaweza kutumikam wka wananchi wa Zanzibar kwa kuanzia na hatimae kupanua soko hadi kwa Tanzania Bara.

Kupata studio zilizo bora za Redio, kuweka mfumo mpya wa umeme na baridi ZBC Televisheni na baadae ZBC Radio na kuwa na vifaa bora na vya kisasa kabisa ambavyo vitakidhi haja ya leo na baadae.

Alieleza kuwa kampuni tatu zilitoa huduma ya ujenzi, kuuza vifaa, ufungaji wa vifaa pamoja na kutoa mafunzo ambazo ni Kampuni ya DV International Group ya Ufaransa, ABV International Company ya Singapore na Kampuni ya Fortune four kutoka Jamhuri ya Czech.

Alisema kuwa mradi huo wa matengenezo ya studio mpya pia, yalihusisha moja kwa moja na uimarishaji wa Kampuni ya ZMUX, hivyo hafla hiyo inaendana na ufunguzi wa mitambo ya kusambaza na ufunguzi wa mitambo ya kusambaza maudhui ya ZMUX zilizopo Rahaleo ambapo pia studio tatu zimewekekwa vifaa vya kisasa ambapo gharama zake zote kwa pamoja ni TZS Bilioni 4.7 pamoja na gharama za usimamizi zitakuwa TZS Bilioni 5.3 ambazo zote zimetolewa na SMZ.

Katibu Mkuu huyo alieleza kuwa kutokana na utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 ulivyofanyika itakapofika 2020 au kabla ya hapo itakuwa Ilani hiyo itakuwa imekamilika.

Mapema Dk. Shein alikagua studio hizo mpya katika jengo hilo la Karume House pamoja na kupata maelezo kutoka kwa wataalamu wazalendo pamoja na wataalamu kutoka kampuni za nje ya Zanzibar zilizofanya kazi ya kuingarisha na kuziwekea vifaa stuo hizo

**Rajab Mkasaba, Ikulu Zanzibar**

**Postal Address: 2422 Tel.:0777427449. Fax: 024 2231822**
**E-mail: rajabmkasaba@yahoo.co.uk**